

Mradi wa ASCENT unawasaidia wagonjwa kuwa na ufuasi mzuri wa matibabu kwa kutumia teknolojia ya kidigitali kama vile sanduku maalumu la kidigitali au bahasha maalumu za dawa za TB.

# ASCENT: WEZESHA WAGONJWA KWA KUTUMIA TEKNOLOJIA YA KIDIGITALI YA UFUASI MZURI WA MATIBABU

**Mradi wa ASCENT unaofadhiliwa na shirika la Unitaid unalenga kusaidia wagonjwa kufanikiwa kumaliza matibabu ya TB kwa kutumia teknolojia ya kidigitali ya ufuasi mzuri wa matibabu.**

Kifua Kikuu (TB) bado ni ugonjwa hatari wa kuambukiza unaosababisha vifo vingi zaidi kote ulimwenguni. TB husababisha zaidi ya vifo vya watu 4.000 kila siku. Vifo hivi havikuwa na sababu ya msingi kwa kuwa TB inatibika na kupona kabisa. Aidha kuna vikwazo kadhaa vinavyowafanya wagonjwa washindwe kupona ugonjwa huu, ikiwa ni pamoja na urefu wa muda wa matibabu, changamoto za wingi wa aina za dawa za kunywa kila siku kwa kipindi cha miezi 6 mpaka 24. Kutokunywa dawa kwa siku chache au kuacha kuendellea na matibabu kuna weza kusababisha usugu wa dawa au kurudiwa na ugonjwa siku za usoni baada ya kupona.

Hivyo, wagonjwa mara zote wanahitaji kunywa dawa kila siku chini ya usimamizi kwa kwenda kwenye kituo cha tiba au kwa mhudumu wa afya kwenda nyumbani kwake. Ni wazi kuwa aina hii ya usimamizi unaongeza mzigo sio tu kwa mgojwa bali pia katika mfumo mzima wa kutoa huduma za afya. Kwa kuwekeza katika maendeleo ya sasa ya teknolojia ya habari na mawasiliano (simu za kiganjani), mradi wa ASCENT ("Adherence Support Coalition to End TB") unalenga kuwawezesha wagonjwa wa TB kuendelea na matibabu yao kwa njia ya kisasa na yenye ufanisi zaidi. Kwa kukusanya ushahidi, kutengeneza uhitaji wa kimataifa na kushirikisha wadau wengine wa maendeleo, ASCENT inalenga kuwezesha usambazwaji ambao utafanya ubunifu huu wa kidigitali kupatikana kwa wagonjwa wote wa TB dunia nzima.

## Fikiri kutoa huduma bora zaidi

**Mradi wa ASCENT unawasaidia wagonjwa kukamilisha matibabu yao kwa ufanisi kupitia matumizi ya teknolojia ya kidigitali ya ufuasi mzuri wa matibabu ambao ni afua inayozingatia matumizi sahihi ya takwimu, vifaa vya kisasa kama masunduku ya kidigitali ya dawa na ubunifu mwingine.**


**Mfumo huu wa kidigitali unamwezesha mgojwa kutumia dawa zake za kila siku kwa muda na sehemu ambayo ni muafaka kwake zaidi.**

**Mpaka sasa, teknolojia hii inatumiwa kwa kiasi kidogo kwenye mapambano dhidi ya TB kimataifa. Mradi wa ASCENT unalenga kuifanya ipatikani kwa wagonjwa wote wa TB kote dunia.**

## Mifano ya faida kwa wagonjwa:



**Mgonjwa ana uwezo wa kuchagua wapi pa kunywea dawa. (mf. Nyumbani)**



**Mgonjwa anaweza kutumiwa ujumbe mfupi kupitia simu ukimwelekeza kufanya jambo fulani. (mf. Kukumbushwa kunywa dawa/ kwenda kumwona daktari)**



**Wagonjwa wanapokea ujumbe mfupi unaoendana na aina ya matibabu anayopokea kupitia simu za kiganjani.**

## Mifano ya faida kwa watoa huduma:




**Kupitia mfumo, mtoa huduma anapata taarifa za ufuasi wa kila mgonjwa kwa wakati.**




**Mfumo unaweza kuwatumia ujumbe au taarifa ya hali ya ufuasi wa wagonjwa wao hili kuchukua hatua stahiki.**



**Mfumo unao uwezo wa kuchakata taarifa za ufuasi na kubaini wagonjwa ambao wanahitaji ufuatiliaji wa karibu/msaada zaidi.**

---

ascent
Adherence Support Coalition to End TB

# Teknolojia ya kidigitali ya ufuasi mzuri wa matibabu

Mradi wa ASCENT utatekeleza na kutathmini aina tatu tofauti ya mifumo ya kidigitali ya ufuasi mzuri wa matibabu itakayopatikana bila malipo katika vituo ambavyo washiriki wanapatiwa huduma za afya. Mtoa huduma za afya ataelezea namna ya kutumia teknolojia hizi kama sehemu ya huduma za kawaida wanazopatiwa wagonjwa wakati wa kuanzishiwa matibabu.

## 1: Bahasha maalumu za dawa

Mgonjwa atapokea dawa zake za TB zikiwa kwenye kifungashio maalumu. Kila siku, mgonjwa atapiga simu ya bure au kutuma ujumbe mfupi kuonyesha amekunywa dawa siku hiyo.


## 2: Sanduku la kidigitali la dawa

Mgojwa atapewa sanduku maalumu lililotengenezwa kwa ajili ya kuhifadhi dawa zao za TB. Kila mara mgonjwa atakapofungua sanduku hili, kifaa maalumu kilichowekwa kwenye sanduku hilo kitatuma taarifa na kumjulisha mtoa huduma kuwa mgonjwa amekunywa dawa siku hiyo.

## 3: Usimamizi wa matibabu kwa video

Wakati wa kunywa dawa, mgonjwa atajichukua picha ya video kwa kutumia program tumishi kwenye simu yake. Baada ya kumaliza, video hiyo inatumwa kwenda kwa mtoa huduma kwa ajili ya uhakiki.


1




2



3




## Wadau

Kupitia muunganiko thabiti wa umoja wa wadau (KNCV Tuberculosis Foundation, The Aurum Institute, London School of Hygiene & Tropical Medicine na PATH) kwa ushirikiano na serikali ya Tanzania, mradi wa ASCENT utachangia ukubalikaji na matumizi ya teknolojia ya kidigitali ya ufuasi mzuri wa matibabu. Mradi wa ASCENT umewezekana kwa msaada na ufadhili wa shirika la Unitaid.




Mradi wa ASCENT utakaotekelezwa kuanzia Julai 2019 mpaka Disemba 2022 unalenga kuwafikia takribani wagonjwa 70,000 kutoka Ukraine (1), Ethiopia (2), Tanzania (3), Afrika Kusini (4) na Ufilipino (5)

**Utazingatia:**

- Kuwezesha nchi kiteknolojia ya kidigitali ya ufuasi mzuri wa matibabu.
- Kutoa ushahidi mahususi juu ya matumizi na namna bora ya usambazaji.
- Kuhamasisha soko la kimataifa na mpango wa utekelezaji wa teknolojia ya kidigitali ya ufuasi mzuri wa matibabu.

**Mawasiliano:**

www.digitaladherence.org
ascent@kncvtbc.org

Unitaid Innovation in Global Health | KNCV TUBERCULOSIS FOUNDATION | PATH | THE AURUM INSTITUTE | LONDON SCHOOL of HYGIENE &TROPICAL MEDICINE